

FASIHI ANDISHI YA KISWAHILI NA DINI: MIFANO YA RIWAYA ZA SAID AHMED
MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI

Miriam Osore
Idara ya Kiswahili
Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya
kenyanimo@yahoo.com

Ikisiri

Wataalamu wengi kama Ngugi wa Thiong’o na Alter (1981) wanaona kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya itikadi ya kidini, maandishi ya kidini na utunzi wa fasihi. Hii inamaanisha kwamba watunzi wa kazi za kubuni hurejelea maandishi ya kidini kama Korani na Biblia. Ngugi wa Thiong’o katika hotuba yake ya kongamano la 57 la Baraza la Kitaifa la Mekanisa Nchini Kenya (57th National Council of Churches of Kenya), anadhihirisha msimamo huu. Anataja kwamba “katika Afrika, jinsi ilivyo katika maeneo mengine duniani, Biblia ndilo andiko la kimsingi la fasihi za mataifa mbalimbali” (*East African Standard*, Alhamisi tarehe 26^h, Agosti 2004:7). Tamko hili la Ngugi linamaanisha kwamba kuna mwingiliano matini kati ya Biblia na kazi za fasihi za mataifa mbalimbali. Kwa upande wake, Alter anaeleza kwamba maandishi wa Biblia wametumia ubunifu wa hali ya juu. Makala haya yanalenga kubainisha ni kwa kiwango na jinsi gani Mohammed na Kezilahabi wameathiriwa na dini ya kiislamu na kikristo mtawalia katika riwaya zao. Vilevile yatadhihirisha mwingiliano wa matini unaodhihirika kati ya dini hizi na utunzi wa riwaya za maandishi hawa.